MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA MAALUM LA MADIWANI ULIOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA TAREHE 29/09/2017 KWA AJILI YA KUFUNGA HESABU KWA MWAKA UNAOISHIA JUNI, 2017

A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

1.	" Jamal M Mtima	-Kata ya Namikupa	-Mwenyekiti
2.	" Issa Nasoro Kalumbe	-Kata ya Mahuta	Mjumbe
3.	" Ngerezani Bakari Musa	-Kata ya Kitama	"
4.	" Kawasaki Lipangati	-Kata ya Mnyawa	"
5.	" Simba Nasoro Hashimu	-Kata ya Naputa	"
6.	" Chimale S. Abdallah	-Kata ya Lukokoda	"
7.	" Sharafi Dihoni Hamisi	-Kata ya Malopokelo	"
8.	" Mtimbuka K.Ramandani	-Kata ya Nambahu	"
9.	" Mawazo S. Mbombenga	-Kata ya Nanhyanga	"
10.	" salumu Makuyeka	-Kata ya chikongola	"
11.	" Ally D. Nantindu	-Kata ya Michenjele	"
12.	" Nembo H. Mchola	-Kata ya Maundo	"
13.	" Ahmadi A. Ndende	-Kata ya Mkoreha	"
14.	" Ashura m. Ngope	-Kata ya Mchichira	"
15.	" Mohamedi T. Ussi	-Kata ya Kwanyama	"
16.	" Selemani Y. Chambengela	-Kata ya Litehu	"
17.	" Ismail S. Chipoka	-Kata ya Ngunja	"
18.	" Zainabu H. Mpota	-Kata ya Mkonjowano	"
19.	" Alafa T. Nakatanda	-Kata ya Mkwiti	"
20.	" Ayubu Mohamedi	-Kata ya Lyenje	"
21.	" Rashidi N. Mtima	-Kata ya Chingungwe	"
22.	" Mfaume H. Abdallah	-Kata ya Miuta	"
23.	" Mkwahe M. Milembu	-Kata ya Chaume	"
24.	" Salumu A. Mnyongo	-Kata ya Dinduma	"
25.	" Abdallah H. Ponela	-Kata ya Luagala	"
26.	" Likapa J.Nangololo	-Kata ya Mndumbwe	"
27.	" Hamisi B. Nayowela	-Kata ya Tandahimba	"
28.	" Fakihi M. Mwango	-Kata ya Mdimba	"
29.	" Yusufu B. Nampoto	-Kata ya Mkundi	"
30.	" Asha R. Tebwa	-Viti Maalum	"
31.	" Halima Tamatama	-Viti Maalum	"
32.	" Huduma S. Mnoda	-Viti Maalum	"
33.	" Amina Issa Mpota	-Viti Maalum	"
34.	" Hadija S. Mnihwika	-Viti Maalum	"
35.	" Shamia M. Kaisi	-Viti Maalum	"
36.	" Fidea A. Hittu	-Viti Maalum	"
37.	" Asia A. Likoba	-Viti Maalum	"
38.	" Rehema C. Liute	-Viti Maalum	"
39.	" Hawa M. Ramandani	-Viti Maalum	"

40. Mhe. Amina A. Simba -Viti Maalum "

B: WASIOFIKA

1. Mh. Namkulya S. Namkulya -Kata ya Mihambwe -Kwa Taarifa
2. " Katani A. Katani -Mbunge- Tandahimba -Kwa taarifa
3. " Ramadhani Ulaya -Kata ya Milongodi - Amefariki

C:WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA:

1. Ndg Ahmada Suleiman- Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W) Katibu
2. Ndg. Lazaro Matoke -Kaimu Afisa Utumishi (W)
3. " Machela A.H -Mweka Hazina (W)
4. " Issa Naumanga -Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika (W)
5. " Bakari Njunju -Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)
6. Eng: Peter Malekia - Mhandisi wa Maji (W)
7. Dr. Antipas Swai -Mganga Mkuu (W)
8. " Laura N. Daudi -Kaimu Afisa Ardhina Maliasili(W)
9. " Robert Mwanawima -Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
10. " Sosteness Luhende -Afisa Elimu Sekondari (W)
11. " Kashen Mtambo - Kny: Afisa Mipango (W)
12. " Viktor Mkusa -Kaimu Mkaguzi wa ndani wa Hesabu(W)
13. " Rajabu Lwazi -TEO- Mahuta
14. " Nosyaga Mwailunga - Kaimu Afisa Usafi na Mazingira(W)
15. " Rajabu C. Athman -Afisa Utamaduni
16. " Martha Sinkamba -Kaimu Afisa Elimu msingi(W)
17. " Zuberi Sarahani -Mwanasheria
18. " Protas Muhanuzi -Afisa Manunuzi(W)
19. " Ismail Mbilinyi -Mratibu wa TASAF
20. " James C. Chitumbi -TEO Tandahimba
21. " Sood Rajabu - Afisa Ushirika
22. " Geofrey Rutakinikwa - Afisa Utumishi
23. " Christina Damiana - Mhasibu
24. " Violeth Mahembe - Mratibu wa CHF

D: WAALIKWA

1. Mh. Sebastian Waryuba -Mkuu wa Wilaya Tandahimba
2. Ndg: Mohamedi Azizi - Katibu Tawala (W)
3. " Juma A. Lusasi -Afisa Tarafa Mahuta
4. " Rehema Hoza -Afisa Tarafa Litehu
5. " Born Minga -Afisa Tarafa Namikupa

E: SEKRETARIATI

1. Christian Mazuge
2. Doris Jeremiah

MUHT.NA. 04/2017/2018- KUFUNGUA MKUTANO

Katibu aliwakaribisha wajumbe,Watendaji na Wageni waalikwa kwenye kikao hicho na kueleza kuwa ni kikao maalum cha kujadili taarifa ya kufunga Hesabu za Halmashauri kwa mwaka unaoishia Juni 2017.

Baaday ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alifungua kikao saa 4:59 asubuhi.

MUHT.NA. 05/2017/2018 - TAARIFA YA FEDHA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30, JUNE 2017.

Mweka Hazina (W) aliwasilisha taarifa ya fedha za Halmashauri ya Wilaya Tandahimba kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2017 kama ifuatavyo:-

Mizania ya mwaka 2016/2017

Mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka 2016/2017 rasilimali za Halmashauri za muda mrefu na mfupi zilikuwa na thamani ya jumla ya **Sh. 37,628,690,036/=** wakati dhamana na dhima ya muda mrefu na mfupi ilikuwa na thamani ya **Sh. 10,432,446,128/=.** Ongezeko la rasilimali za Halmashauri limetokama na Halmashauri kutekeleza miradi mbalimbali yenye mwelekeo wa rasilimali za kudumu pamoja na ununuzi na ujenzi wa miundombinu.

Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka 2016/2017

Halmashauri ilikusanya kutoka vyanzo vyake vya Ndani (own source) na vile vya ruzuku Jumla ya **sh. 31,092,068,711/=** na kutumia **sh. 28,071,144,702/**= kwa matumizi ya mishahara na matumizi ya kawaida.

Mtiririko wa fedha kwa kuanzia kiwango cha ziada/albaki ya mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 ilikuwa kama ifuatavyo:-

- Alibaki ya fedha kutokana na uendeshaji 2,820,213,171
- Fedha zilizotokana na uwekezaji (3,766,042,012)
- Fedha kutokana na ufadhili 373,439,102
- Punguzo la fedha kwa mwaka 2016/2017 (572,389,739)
- Salio/Bakaa iliyokuwepo benki tarehe 1/7/2016 1,560,592,056
- Salio/Bakaa iliyokuwepo benki tarehe 30/6/2017 988,202,318

MAELEZO YA HALI YA FEDHA

MIZANIA

1. Fedha taslimu:

Fedha taslimu imepungua kutoka **Sh 1.560** billion mwaka 2016 mpaka **Sh 0.998** billioni 2017 ikisababishwa na uwekezaji wa nyuma.

2. Wadaiwa

Wadaiwa wameongezeka kutoka **Sh.2,046,983,584/=** mwaka 2016 mpaka **Sh. 3,064,698,073/=** mwaka 2017. Hii imesababishwa na kuongezeka kwa mikopo ya vikundi vya vijana na wanawake, hata hivyo hakukuwepo na baadhi ya vyama vya msingi na kutolipa ushuru wa zao la korosho na kulingana na mauzo na madeni ya mikopo ya wanawake na vijana.

3. Mali ghalani.

Mpaka tunafunga hesabu za mwisho kulikuwepo na mafuta, madawa, vifaa vya ofisi na shajala stoo katika maghala ya Halmashauri kwa pamoja vikiwa na thamani ya **Tsh. 304,707,664**/=.

4. Rasilimali zinginezo

Halmashauri ilikuwa na amana ya muda mrefu ambayo imebakiza chini ya miezi kumi na miwili kuiva katika benki ya wananchi Tandahimba yenye thamani ya **sh**. **75,600,000/=** na hivyo kufanya jumla ya rasilimali zinginezo kuwa **sh. 293,141,300/=**

5. Kitega uchumi cha ushirikiano (Investments in associates)

Halmashauri imewekeza **Tsh. 453,686,046** kwa kununua hisa kwenye benki ya wananchi Tandahimba **(TACOBA).** Hakukuwa na ongezeko la hisa za Halmashauri katika benki hii.

6. Majengo, mitambo na Vifaa:

Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri imefanikiwa kuongeza majengo, mitambo na vifaa kwa kiasi cha **Sh 3,766,042,012/=** ambazo zimetokana ruzuku toka serikali kuu na na mapato ya ndani.

7. Wadai (payables)

Wadai waliongezeka kutoka **Tsh. 207,420,581** mwaka 2015/2016 hadi **Tsh 227,343,228** mwaka 2016/2017

B: MAPATO

1. Kodi-Ushuru wa mazao:

Mapato kutokana na kodi mbalimbali kama ushuru wa mazao yameongezeka kutoka **Sh 3,395,868,925/=** mwaka 2015/2016 mpaka **Sh 5,651,892,460** kwa Mwaka 2016/2017 kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la korosho pamoja na bei dira ya korosho.

2. Ada, faini, adhabu na leseni

Mapato kutokana na vyanzo hivi yameongezeka kutoka **Sh. 157,985,914/=** mwaka 2015/2016 mpaka **Sh. 399,299,762/=** mwaka 2016/2017,

3. Ruzuku ya kawaida

Mapato yanayotokana na fedha za ruzuku zilizotoka serikalini kwa matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka **Shs. 23,880,860,1991/=** kwa mwaka 2015/2016 mpaka **Shs. 23,903,529,906/=** mwaka 2016/2017.. imechangiwa na ongezeko la fedha za kaya masikini**(TASAF)** pamoja na fedha za elimu bure kwa shule za msingi na sekondari.

4.Mapato yanayotokana na ukodishaji/kupangisha/kuuza nyumba za Halmashauri.

Mapato yanayotokana na vyanzo hhivi yanategemea sana ukodishaji wa lori la Halmashauri, upangishaji wa nyumba za watumishi,sehemu ya jengo la ukumbi wa Halmashauri (CRDB) na uuzaji wa mali za Halmashauri(Disposal). Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri haikuuza mali zake hata hivyo mapato yalifikia kiasi cha **sh. 19,170,000/=**

5. Thamani ya rasilimali zilizotumika

Hii ni sehemu ya uchakavu wa majengo, mitambo na vifaa ambayo inajumuishwa kama sehemu ya mapato kwa kila mwaka baada ya kutumika hiyo rasilimali Kwa mwaka 2016/2017 thamani ya rasilimali iliyotumika ilikuwa **Sh 1,375,465,775.**

C: MATUMIZI

1. Mishahara na Maslahi ya watumishi.

Malipo ya mishahara na maslahi ya watumishi yamepungua kutoka Sh **20,338,108,054** mwaka **2015/2016** mpaka sh **19,605,783,969.**

2. Ununuzi wa vifaa na gharama za kujikimu kwa wafanyakazi

Ununuzi wa vifaa na gharama za kujikimu kwa watumishi umeongezeka kutoka sh. **2,339,482,424** mwaka **2015/2016** mpaka sh. **3,476,444,022 mwaka 2016/2017 ikiwa nitofauti y ash. 1,136,953,798.**

3. Gharama za matengenezo

Matumizi ya gharama za matengenezo ni pamoja na matengenezo ya barabara na magari na ununuzi wa mafuta ya kuendeshea mitambo, magari na pikipiki ambayo yameongezeka kutoka sh. **934,994,727** mwaka **2015/2016** mpaka sh. **1,420,260,916** mwaka **2016/2017**. Ikiwa ni ongezeko la shilingi 485,686,189.

4. Ruzuku na michango ya kuchangia jamii

Kiasi kimeongezeka kutoka kutoka sh **1,782,194,325** mwaka **2015/2016** hadi Sh **2,170,023,519.** mwaka **2016/2017**. Hii kwa kiasi kikubwa imetokana na utekelezaji wa miradi ya TASAF.

5. Uchakavu wa mitambo na vifaa

Ni sehemu ya makadirio ya uchakavu wa majengo, mitambo na vifaa kwa mwaka (depreciation expenses). Kumekuwa na ongezeko la sh.

95,077,750(1375,465,775 mwaka 2016/2017 kutoka 1280,388,025 mwaka 2015/2016. kutokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ambayo ilikuwa katika hatua za utekelezaji mwishoni mwa mwaka uliopita na ununuzi wa vitendea kazi vipya.

Taarifa ilipokelewa.

MJADALA

Mjumbe aliomba kujua maana ya kuiva kwa rasilimali **Tshs. 75,600,000/=** iliyowekezwa katika Benki ya wananchi Tandahimba (**TACOBA).**

Mweka Hazina alieleza kuwa fedha hiyo waliwekeza **TACOBA** kwa miaka 2 na itaiva kati ya mwezi Februari na Marchi ,2018.

Mjumbe aliuliza wadaiwa wa vyama vya msingi watalipa lini madeni, mtaalam alishauri kuwa madeni ya muda mrefu Baraza liamue kuyasamehe.

USHAURI

Mjumbe alieleza kuwa suala la wadaiwa lijadiliwe kwenye kikao cha Baraza maalumu. Katibu alieleza kuwa ni vyema jambo hili likajadiliwa katika vikao vya kawaida na Baraza la robo ya kwanza la mwezi Oktoba.

SUALA LA WADAIWA

Mjumbe aliuliza wadai waliotajwa ni akina nani. Ilielezwa kuwa wadai hawa ni watumishi, wazabuni na watoa huduma mbalimbali za Halmashauri.

Suala la Ujenzi wa vyoo S/M Miuta

Diwani wa Miuta alieleza kuwa shule ya Msingi Miuta haikupata shilingi milioni 20 hivyo akaomba kiasi hicho cha fedha kuondolewa kwenye fedha zilizotumika. Mweka Hazina alieleza kuwa hesabu hiyo imeingizwa kimakosa na kueleza kuwa ataondoa kwenye mahesabu.

Mjumbe aliuliza kuhusu ujenzi wa nyumba zahanati ya Mganga wa Maundo. Ilielezwa kuwa nyumba hiyo ni mradi wa SEDP ambayo ilijengwa mwaka 2013 na ilishakamilika na kuanza kutumika.

MUHT.NA. 06/2017/2018 -TAARIFA YA UHAMASISHAJI WA RASIMU YA SHERIA NDOGO ZA VIJIJI

Afisa sheria aliwasilisha rasimu ya uandaaji wa sheria ndogo za vijiji kwa kueleza kuwa asilimia 95 ya vijiji tayari vimewasilisha rasimu ya sheria zilizotungwa na vijiji. Halmashauri imefanikiwa kuandaa aina tatu za rasimu za sheria ndogo kwa kila kijiji ili kukidhi mahitaji yake. Sheria hizo ni:-

(i) Rasimu za sheria ndogo za maendeleo ya Jamii
(ii) Rasimu za sheria ndogo za ada na ushuru.
(iii) Rasimu za sheria ndogo za utunzaji Misitu.

Maeneo muhimu yaliozingatiwa kwenye sheria ndogo.

Katika mchakato mzima wa uandaji wa sheria ndogo za vijiji kuna maeneo muhimu ambayo yametiliwa mkazo kwa mujibu wa mwongozo wa uandaaji sheria ndogo za vijiji wa mwaa 2011 kutoka TAMISEMI. Maeneo hayo ni:-

I. Mipango mbalimbali ya maendeleo inayobuniwa na vijiji husika
II. Michango/tozo mbalimbali kwa ajili ya uanzishaji na uendelezaji wa mipango ya vijiji kupitia mifugo na mazao kama vile korosho na mazao mchanganyiko.
III. Uzuiaji wa kuchoma moto katika maeneo ya vijiji.
IV. Uzuiaji wa wa ununuzi wa korosho usio rasimi "**KANGOMBA"**
V. Uhamizaji wa wanafunzi kihudhuria masomo shuleni.
VI. Adhabu kwa wanaokizana na sheria ndogo za vijiji.

Baadae aliomba mkutano wa baraza tukufu kupitisha sheria ndogo ili zianze kutumika kwenye vijiji vyote.

MJADALA

Mjumbe aliuliza kwa vijiji ambavyo havijaleta ni lini vitaleta rasimu za sheria ndogo? Ilielezwa kuwa mwanasheria atatumia mapendekezo ya 95 kusaidia hata vijiji vingine kutunga sheria.

USHAURI

Mjumbe alishauri sheria ndogo zinazotungwa wataalam wazisimamie kwa makini kwa kuwa kumekuwa na changamoto ya vyama vya msingi kufungua matawi(vikonyo) kwenye vijiji vingine.

Swali:-

Mjumbe aliuliza rasimu hizo zimeandaliwa na nani?
Mjumbe aliuliza ukomo wa eneo la kununua korosho kwa vyama vya msingi.

Jibu
Afisa Ushirika alieleza kuwa sheria ya Ushirika inaposajili chama inatoa cheti. Inatoa mipaka ya kufanya kazi na mipaka ya kazi sio kijiji wala kata bali ni eneo ambalo chama kinatoa huduma kwa wanachama wake.

SUALA LA CHAKULA
Mwenyekiti alionyesha kusikitika kukosa huduma ya chakula wakati wa vikao vinapofanyika jambo ambalo linawafanya kupeleka mambo haraka ili kuwahi kumaliza.

AZIMIO

1. Kikao kiliazimia kuwa huduma ya chakula lazima itolewe kwenye vikao vya kamati.

Mwenyekiti alieleza kuwa katika kusimamia zao la korosho zinazouzwa kwenye vyama vya msingi wajumbe wa kikosi kazi wajikite kuzuia kutoroshwa korosho gafi nje ya mipaka ya wilaya ya Tandahimba.

SUALA LA MAGUNIA.
Ilielezwa kuwa kuna gunia million 1.5 zimefika ila kuna kazi ya kupiga chapa na kuhofia kuwa upigaji chapa ukichelewa utasababisha wakulima kukosa magunia na kumuomba Mkuu wa Wilaya kufuatilia kwa kwenda kujionea mwenyewe na kuwasilisiana na bodi ya korosho.

NASAHA ZA KATIBU TAWALA (W)
Katibu Tawala(W**)** Alitoa taarifa za ujio wa Waziri Mkuu wa Jauhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kasimu Majaliwa tarehe 07/10/2017.

NASAHA ZAMKUU WA WILAYA
Mkuu wa wilaya alieleza kuwa alikuwa na wageni wa aina mbili

(i) Ugeni wa Waziri Mkuu
(ii) Ujumbe wa wadau wanaofuatilia madeni ya pembejeo

Alieleza kuwa sheria ndogo zinazotengenezwa hazitakiwi kukinzana na sheria ndogo za Halmashauri na sheria za Nchi.

SUALA LA UNUNUZI HOLELA WA KOROSHO (KANGOMBA)

Mkuu wa Wilaya aliwashukuru Madiwani na wakuu wa Idara na Vitengo kwa kushirikiana katika kuzuia kangomba msimu wa 2016/20017.

Alieleza kuwa katika msimu 2017/2018 hataki ununuzi wa korosho nje ya chama ufanyike. Alieleza kuwa vyama vya msingi vitafanya kazi kwenye maeneo yake kwa mujibu wa sheria kama ilivyoelezwa wakati wa usajili.

SUALA LA MAGUNIA

Mkuu wa Wilaya alisema kuwa kwa mwaka huu magunia yana rangi zinazotofautiana katika wilaya moja hadi nyingine kwa lengo la kuzuia utoroshaji wa korosho na suala la ucheleweshaji wa magunia atalifuatilia.

MUHT.NA. 07/2017/2018- KUFUNGA MKUTANO

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao.

Mwenyekiti alieleza kuwa Katibu Tawala (M) anahitaji wanafunzi wenye ufaulu wa kidato cha nne kwa ufaulu usiopungua alama D. nne. Pia alieleza kuwa Tarehe 26/09/2017 kulifanyika uzinduzi wa zoezi la usajili wa watoto wenye umri chini ya miaka 5, hivyo kuomba kuhamasisha wananchi kujitokeza na kujiandikisha, baada ya maelezo hayo alifunga kikao saa 7: 54 mchana.

MUHTASARI UMETHIBITISHWA NA

JINA _____ **JINA** _____

MWENYEKITI **KATIBU**

SAINI _____ **SAINI** _____

_____

TAREHE